FIDIA KWA AJILI YA BARUA PEPE, SIMU NYARAKA ZILIZOKAGULIWA NA MALIPO YA HUNDI KWA MTU MWINGINE

KWA KUWA Mimi/Sisi tuliotia saini_____(jina la mmiliki akaunti) na _____(jina la mmiliki akaunti) tumeomba na kuidhinisha Benki ya Stanbic Tanzania ("Benki", "sisi" au "wewe") kuchukua hatua kuhusu maelekezo au mawasiliano yoyote yaliyofanywa na mimi/sisi kwa madhumuni yoyote, ambayo yanaweza mara kwa mara kuwa au kuchukuliwa kutolewa kwa njia ya barua pepe (kumbukumbu zozote kuhusu "barua pepe" katika mamlaka haya na fidia itakuwa na maana ya kila maagizo yaliyotiwa saini na kupelekwa kwa Benki ambayo imeambatishwa kwenye barua pepe).

NA KWA KUWA Mimi/Sisi tunakubali kuwa maelekezo ya faksi na/au ujumla wa barua pepe sio njia za mawasiliano zisizo na makosa na tunakubali kuwa sio rahisi kwa Benki kuthibitisha usahihi wa ujumbe wote uliotumwa kwa barua pepe au skani pia kuwasilishwa kwa njia ya simu kwa Benki ikidaiwa kutoka kwangu/sisi;

NA KWA KUWA Benki imetuarifu mimi/sisi kwamba iko tayari kuchukua hatua kuhusu maelekezo yawe yametumwa kwa baruapepe/nyaraka zilizokaniwa) au kwa simu ambazo zinadaiwa kutoka kwangu/sisi ili ipate fidia katika fomu iliyokamilishwa.

NA KWA KUWA mimi/sisi tuko tayari kutoa fidia hiyo:

KWA HIYO BASI mimi/sisi hapa:

1. Nakubali kuwa maelekezo yote, yawe ujumbe wa barua pepe, nyaraka zilizokaguliwa, wakilishi ridhaa, ahadi na nyaraka nyingine zinazodaiwa kutoka kwangu/sisi zitachukuliwa kutolewa na mimi/ sisi katika namna ambayo imepokelewa na Benki (maelekezo kwa barua pepe au waraka uliokaguliwa) ambayo inaweza, kutokana na uharibifu wa kifaa, upotoshaji wa mawasiliano, na aina yake, yanaweza kuwa tofauti na ile iliyokusudiwa au kupelekwa na mimi/sisi tutawajibika nayo;

2. Achia haki zozote ambazo mimi/sisi tungeweza kuwa nazo au kuzipata sasa hivi au baadaye dhidi ya Benki kutokana moja kwa moja au sio moja kwa moja kutokana na hasara yoyote au uharibifu ambao mimi/sisi tunaweza kuupata kwa kuwa Benki (kwa jumla au sehemu) inachukua hatua kuhusu maelekezo yoyote ya barua pepe au yaliyokaguliwa au kwa njia ya simu pamoja na kumruhusu mtu mwingine kuchukua fedha kutoka akaunti yangu/yetu na mimi/sisi tunakubali kuifidia Benki kuhusiana na madai yoyote, malalalmiko au vitendo dhidi yake au hasara au madhara yaliyotokea au kupatiwa na Benki na ambayo yatakuwa yamepatikana ama moja kwa moja au vinginevyo kutokana na kuhusiana na Benki kukubali maelekezo ya simu, yaliyokaguliwa au kwa barua pepe na kuyafanyia kazi;

3. Nakubali kuwa Benki haitahusishwa na makosa au ucheleweshaji katika mawasiliano au kutoeleweka wakati wa upokeaji,au kwa aina yoyote ya hasara au uharibifu kutokana na sababu yoyote kutokana na Benki kuruhusu mpango huu, pamoja na zile nyakati ambapo mimi/sisi tunatumia mwakilishi na au ujumbe kutenda kwa niaba yetu katika ukusanyaji fedha kutoka Benki isipokuwa hasara inayotokana na vitendo kinyume na sheria au udanganyifu vilivyothibitishwa vya watumishi wa benki;

4. Nakubali kutekeleza na kufuatisha taratibu zozote na/au makatazo yaliyowekwa dhidi yangu/sisi na Benki mara kwa mara kuhusiana na upelekaji wa maelekezo Benki au watu wengine wanaotekeleza wajibu huu kwa niaba yangu/sisi;

5. Nakubali kuwa mimi/sisi; tunawajibika moja kwa moja kwa na kuwajibika kwa vitendo kuhusu malipo ya hundi katika akaunti yangu/yetu. NA KWA KUWA, Benki imeniarifu/imetuarifu kwamba iko tayari kuchukua hatua kuhusiana na maelekezo yetu kama ilivyotajwa hapo juu;

6. Nakubali kuwa fidia hii haitaathiriwa na kushindwa kwa Benki kuweka taratibu za kutosha au vizuizi kuhakikisha kuwa kimoja wapo au vyote vinatekelezwa;

7. Bila kujali vipengele vyote vilivyopo, Benki kwa ridhaa yake pekee haitalazimika kuchukua hatua kwenye maelekezo yoyote kuhusu barua pepe or waraka uliochunguzwa au kwa njia ya simu pamoja na hundi iliyowasilishwa na mtu mwingine na kwamba kwa nyakati tofauti inaweza baada ya kupata taarifa ya maandishi iliyotumwa kwangu/sisi kwa (sehemu makazi; anuani ya posta, barua pepe, ukaguzi, namba ya simu) kuachana na mipango iliyotarajiwa na waraka huu;

8. Fidia hii inatengua fidia yoyote ya zamani iliyotolewa na mimi/sisi na itatumika kwa faida ya warithi au wahawilishiwa walioruhusiwa kwenye biashara (kadiri itakavyokuwa). Mimi/Sisi tunakubali kuwa masharti ya humu yatabaki na nguvu kamili na utekelezaji isipokuwa pale utakapopokea, na kuwa na muda wa kutosha kuitekeleza, taarifa ya usiitishaji kwa maandishi iliyotiwa saini na mimi/ sisi, isipokuwa usitishaji huo hautaniepusha mimi/sisi kutokana na dhima yoyote chini ya masharti ya fidia hii mintarafu ya kitendo chochote kilichotendwa na wewe kutokana na fidia hii kabla ya kukamilika kwa muda huo.

9. Fidia hii itatafsiriwa na kusimamiwa na sheria za Tanzania.

10. Kwamba ……na/au…….. kama watumiaji wa barua pepe ambao anuani za majina, cheo, simu na barua pepe ziko hapa chini, wataidhinishwa kupeleka maelekezo ya barua pepe kupitia barua pepe.

Jina	Anuani ya barua pepe	Namba ya simu	Saini

Jina	Anuani ya barua pepe	Namba ya simu	Saini

Jina	Anuani ya barua pepe	Namba ya simu	Saini

Imetiwa Saini tarehe ya…….20……..

KWA NA KWA NIABA YA MMILIKI WA AKAUNTI (Kata kama inavyobidi)

Jina: _____ Jina: _____

Saini: _____ Saini: _____

Tarehe: _____ Tarehe: _____